OUKA
The University of Osaka
Institutional Knowledge Archive

| | |
|---|---|
| Title | Kaida na Miiko katika Utamaduni wa Kiswahili |
| Author(s) | Isack, Zainabu Kassu |
| Citation | 外国語教育のフロンティア. 2021, 4, p. 223-233 |
| Version Type | VoR |
| URL | https://doi.org/10.18910/79373 |
| rights | |
| Note | |

*The University of Osaka Institutional Knowledge Archive : OUKA*

https://ir.library.osaka-u.ac.jp/

The University of Osaka

# Kaida na Miiko katika Utamaduni wa Kiswahili

Norms and Taboos in Swahili Culture

ISACK, Zainabu Kassu

**Ikisiri**

Makala hii fupi inazungumzia *Kaida na Miiko katika Utamaduni wa Kiswahili*. Kila jamiii ina seti ya mambo yanayokubalika, yanayofaa kimaadili na ambayo watu huyafanya kwa desturi haya tumeyaita *Kaida* kwa upande mmoja, na kwa upande wa pili kila jamii ina seti ya mambo ambayo si vizuri kuyasema, kuyafanya au hayakubaliki haya yanangukia katika kapu la *Miiko*. Ili kufahamu, kutangamana, kuwasiliana kikamilifu na kuishi vyema na wengine katika jamii fulani ni muhimu sana kuyafahamu na kuzingatia mambo ya kaida na miiko. Makala hii ni mwendelezo wa juhudi za mwandishi katika kuziba mwanya wa rejea juu ya vipengele mbalimbali vya Utamaduni wa Kiswahili na Utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla zinazowalenga wakufunzi na wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya Kigeni.

Keywords: Kaida, Miiko, Utamaduni wa Kiswahili

**Abstract**

This brief article highlights Norms and Taboos in Swahili Culture (*Kaida na Miiko katika Utamaduni wa Kiswahili*). Every culture has a set of things that are considered folkways, social mores, or things that people do as *norms* on one hand, on the other hand, every culture has a set of things that are forbidden to say or do, immoral things which are referred to as *taboos* in this article. It is of utmost importance to understand and comply to norms and taboos in order to interact, communicate well, and live in harmony with the people of any given culture. This article is a continued effort of the author to bridge the gap of available references aimed for both instructors and learners of Swahili as a foreign language and knowledge of African Culture at large.

Keywords: Norms, Taboos, Swahili culture

## 1. Utangulizi

Makala hii imegawanyika katika sehemu 3: Sehemu ya 1 ni utangulizi ambayo inafafanua mpangilio wa makala, lengo la makala na fasili ya mada/dhana muhimu kadiri zilivyotumika katika

makala hii. Sehemu ya 2 inadondoa, kubainisha na kutolea ufafanuzi mambo ya **kaida** na **miiko** kutokana na vipengele mbalimbali vya maisha katika utamaduni wa Kiswahili. Sehemu ya 3 na ya mwisho ni hitimisho; nayo inatoa muhtasari wa makala hii pamoja na mapendekezo ya mwandishi kwa makala zijazo.

### 1.1 Lengo la Makala

Makala hii ni mwendelezo wa juhudi za mwandishi katika kuziba mwanya wa rejea juu ya vipengele mbalimbali vya utamaduni wa Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla zinazowalenga wakufunzi na wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Kama tulivyokwishagusia katika makala zilizotangulia; mtu anapojifunza lugha ya kigeni anajifunza utamaduni wake pia. Hivyo tunahitaji rejea za kutosha zinazoangazia utamaduni wa Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla zinazowalenga makundi husika katika maandiko ya Kiswahili. Makala zilizotangulia zenye mwelekeo huu ni pamoja na: *Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili* (Isack 2018: 105-118), *Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili* (Isack 2019:259-269) na *Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi* (Isack 2020:193-205).

### 1.2 Kaida na Miiko

Kila Utamaduni una seti ya mambo ambayo yanakubalika kama kaida, adabu au upole kwa upande mmoja na seti ya mambo ambayo yanaonekana kama ni mambo ambayo si ya adabu, si ya upole au miiko kwa mujibu wa mila, desturi na utamaduni wa jamii husika.

Katika makala hii tunayafasili mambo ambayo **ni kaida** kama; mambo ambayo yamezoeleka kufanywa na yanachukuliwa kama sehemu ya desturi za watu. Kaida zinajumuisha mambo ambayo **ni adabu/ni heshima** na kutoyafanya ni **si adabu/si heshima** (kukosa adabu/kukosa heshima). Pia inahusu mambo ambayo **ni upole** haya ni yale ambayo ni vizuri kuyafanya, yaani yanaonyesha ukarimu au kuhimiza maisha ya mtu kutangamana vyema na wengine na kinyume chake ni kukosa upole/**si upole**. Kwa upande mwingine mambo ambayo **ni miiko** tunayafasili kama yale ambayo si vizuri kabisa kuyasema au kuyafanya katika desturi za watu wa jamii husika. Na kuyasema au kuyafanya mambo hayo ni kukiuka au kuvunja miiko ya jamii husika. Aghalabu watu wanahofia kuyafanya au kuyasema kwa kuamini yanaweza kuleta laana au tu kutopendezwa kabisa kuyasikia au kuyaona mambo hayo.

## 2. Mambo ya Kaida na Miiko katika Utamaduni wa Kiswahili

Katika sehemu hii tunadondoa mambo kadhaa ya kaida na miiko kutokana na vipengele

mbalimbali vya maisha katika utamaduni wa Waswahili na kubainisha au kutolea ufafanuzi pale inapojuzu juu ya namna kila jambo linavyofikiriwa katika utamaduni wa Kiswahili. Kwa kila jambo tutabainisha ikiwa jambo hilo linafikiriwa kama; **ni kaida/ni adabu** au **ni upole** kwa upande mmoja au **si adabu/ si upole** au **ni mwiko** kwa upande mwingine.

**2.1 Salamu au Maamkizi:**

Kwanza tutazungumzia kuhusu salamu au maamkizi. Katika utamaduni wa Kiswahili **ni adabu** kuamkiana. Maamkizi hayo tunaweza kuyaainisha kwa kuzingatia wakati, rika na urasmi. Kuna *salamu zenye wakati maalum na salamu zisizo na wakati maalum*. Salamu zenye wakati maalum ni kama; *salamu za asubuhi*; "Habari za asubuhi/ Habari za kuamka" /"Umeamkaje?"/ "Umelalaje?", *salamu ya mchana;* "Habari za mchana", *salamu ya jioni;* "Habari za jioni?" pia "Habari za kutwa?"/ "Umeshindaje?" na salamu zote hujibiwa kwa kusema "nzuri" au "salama".

Pia, zipo salamu ambazo hazina wakati maalum kama vile; "Shikamoo" ambayo mtu hujibu "marahaba", "hujambo" nayo hujibiwa "sijambo", "habari gani" au "habari yako" nazo hujibiwa "nzuri/salama" na "mambo" ambayo hujibiwa "poa au shwari".

Pia tunaweza kuzigawa salamu kwa kuzingatia *rika* na *urasmi*: Salamu "shikamoo-marahaba" ni salamu rasmi na kirika ni salamu ya mdogo kwenda kwa mkubwa. Salamu hii hasa inalenga kuonyesha heshima kwa watu waliokuzidi umri mfano; mtoto kwa wazazi au walimu wake, au watu wengine ambao ni wakubwa kwake. Kwa upande mwingine salamu "mambo-poa" si salamu rasmi, aghalabu hutumika kwa vijana au watu walio na rika moja. **Si heshima** kutumia salamu ya "mambo" kwa mtu aliyekuzidi umri au mkubwa wako katika kazi. Salamu zingine aghalabu ni za kawaida, huweza kutumiwa na rika mbalimbali na katika miktadha rasmi na isiyo rasmi. Mfano wa salamu za kawaida ni kama: "Assalamu aleikum- waaleikum salamu" ambayo aghalabu hutumiwa na waumini wa Kiislamu, "habari- nzuri/salama", "hamjambo- hatujambo" n.k

Jambo muhimu la kitamaduni kuhusu salamu au maamkizi ni kuwa watu wanathamini sana salamu/maamkizi. Na watu hutumia muda wao kusalimiana. Salamu huchukuliwa kama mwanzo wa mazungumzo, mwanzo wa urafiki au namna ya kuendeleza urafiki na kudumisha uhusiano mzuri baina ya ndugu, jamaa na watu wanaofahamiana. Kutomsalimia mtu mnayefahamiana ni ishara ya kukosa adabu hasa ikiwa wewe ni mdogo, au ishara ya mahusiano mabaya au magomvi. Ni kawaida kusikia watu wakisema kama fulani na fulani wana magomvi hawazungumzi, hata salamu hawapeani! Salamu ndio kipimo cha msingi cha uhusiano baina ya watu katika jamii ya Waswahili.

Katika utamaduni wa Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla **ni kaida** watu kuulizana mambo mbalimbali binafsi katika salamu kama; habari za nyumbani/shuleni, habari za

kazi au safari, habari za watoto au familia na kadhalika. **Ni kaida** pia kwa salamu kuambatana na kushikana mikono. Hata hivyo, kubusiana au kukumbatiana si sehemu ya utamaduni wa kawaida wa salamu.

### 2.2 Heshima kwa Wakubwa

Kitamaduni ni wajibu kuwaheshimu wakubwa au wazee. Heshima ni dhana pana sana na mambo ambayo yanadhihirisha heshima ni pamoja na kutoa salamu hasa mdogo kwenda kwa mkubwa, kuwasaidia wakubwa, kufuata ushauri au mawaidha ya wakubwa, kuvaa mavazi ya heshima, kutumia lugha nzuri, mtoto kutimiza wajibu wake kwa wazazi n.k. Kwa upande mwingine mambo ambayo **si heshima** ni kama kumjibu vibaya mzazi na hasa mama au kumtendea mambo mabaya, mdogo kumkosoa, kumuaibisha au kumcheka mkubwa, mzee au mzazi na hasa hadharani, kuweka mikono mifukoni au kuvaa kofia (cap) unapozungumza na mkubwa au mzee, kutowasalimia wakubwa n.k.

### 2.3 Uhusiano Mzuri

Ni wajibu kuwa na uhusiano mzuri na kushirikiana kwa hali na mali na nduguzo, jamaa na hata majirani zako. Hii ni pamoja na kusaidiana kifedha, kusaidiana katika kazi za kijamii, kushirikiana wakati wa furaha kama harusini na wakati wa maafa, misiba au majonzi. Na kutokufanya hivyo ni kukiuka kaida/ **si kaida** na aghalabu huwa chanzo cha mahusiano mabaya, na huleta kutokuelewana baina ya wanajamii.

### 2.4 Ukarimu kwa Mgeni

**Ni kaida** kumkaribisha mgeni chakula au kinywaji. Mgeni ni mtu anayestahili kukirimiwa anapokuja nyumbani kwako. Kwa upande mwingine **si upole** kwa mgeni kukataa chakula au kinywaji anapokaribishwa. Ni bora kula au kunywa japo kidogo (sunna) ili kutomfadhaisha mwenyeji wako.

### 2.5 Chakula

Kipengele cha chakula kimezungumziwa kwa kirefu zaidi katika makala iliyotangulia; *Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi* (Isack 2020: 200-202). Hapa tutarudia kutaja kwa muhtasari tu juu ya mambo ya adabu na miiko ya chakula katika utamaduni husika. Kwanza, **si adabu** kubakisha chakula unapokula au kuchezea chakula. Pili, **ni mwiko** kunusa chakula, kunusa chakula huchukuliwa kama mfano wa wanyama wafanyavyo kabla ya kukila kitu. Tatu, **ni mwiko** kula nyama ya nguruwe (kitimoto) na kunywa

pombe, na kula nyama isiyochinjwa kihalali kwa Waislamu. Nne, **si adabu** kutumia mkono wa kushoto unapokula, kumpa au kupokea chakula kutoka kwa mwingine. Zaidi, **ni heshima** kuwapisha wakubwa au wageni kwanza wakati wa chakula. Mwisho, **si adabu** kutoa sauti wakati wa kula au kuzungumza na chakula mdomoni.

### 2.6 Kubisha Hodi!

**Ni adabu** kubisha hodi! au kupiga hodi! unapoenda nyumbani kwa mtu au ofisini hata pale unapokuta mlango upo wazi. Kubisha hodi! ni kugonga mlango agh. mara tatu "ngo ngo ngo" au kusema maneno kama "hodii!", "hodii wenyewe mpo?" n.k. Kubisha hodi! kuna maana ya kuomba ruhusa ya kuingia au kumtahadharisha aliye ndani kama kuna mgeni. Hata hivyo **si kaida** kubisha hodi sehemu za umma au mahali pa biashara kama mkahawani, dukani, sokoni n.k.

### 2.7 Ishara za Mwili

Ishara za mwili zina maana na ni namna ya mawasiliano kama ilivyo kwa maneno ya lugha. Ishara za mwili huweza kutumika zenyewe au kwa kuambatana na maneno ya lugha. Maana ya ishara nyingi za mwili si majumui (universal) bali ni za kitamaduni. Na hakuna ishara sahihi au zisizo sahihi jambo la msingi ni kuwa ishara hufungamana na utamaduni wa jamii husika. Hivyo ni muhimu kujifunza maana ya ishara kwa kuzingatia utamaduni wa watu wa mahali husika. Ishara moja inaweza kuwa na maana chanya (nzuri) katika utamaduni mmoja, na ikawa na maana hasi au isiwe na maana kabisa katika utamaduni mwingine.

Katika sehemu ifuatayo tutadondoa baadhi ya ishara za mwili katika utamaduni wa Kiswahili na maana au taswira ya kila moja kwa kuzingatia zile zenye maana chanya au zinazokubalika na zile ambazo ni hasi; si adabu au hazikubaliki kitamaduni.

#### 2.7.1 Ishara Chanya

Sehemu hii inaorodhesha baadhi ya ishara ambazo **ni kaida** yaani zinakubalika na hutumika kwa desturi kuashiria maana fulani;

- *Ndiyo*: Kutikisa kichwa juu na chini kunaashiria kukubali.
- *Hapana*: Kutikisa kichwa kulia na kushoto huashiria kukataa, hii pia ni ishara ya masikitiko.
- Njoo: Kukunja vidole vinne kwa pamoja kwa mwendo wa kutoka nje kuja ndani ya kiganja: ni kuashiria kumwita mtu; "njoo". Hasa hutumika tunapomwashiria mtu aliye mbali kidogo aje bila kupaza sauti "njoo".
- *Nenda*: Kutumia vidole vinne vya kiganja katika mwendo kuelekea nje, ni kumwashiria mtu "nenda".

- *Dole*: Kuinua kidole gumba juu maarufu kama ishara ya "dole" ukiwa umekunja vidole vidole vinne vilivyosalia (thumbs up) hii ni ishara chanya ina maana ya "sawa", "-zuri". Nchini Tanzania, ishara hiyo pia ni alama ya chama cha Mapinduzi, CCM. Kwa kulinganisha ishara hii kwa upande mwingine haina maana chanya katika tamaduni nyingine kama nchini Irani na Iraki. Kwa mfano nchini Irani ishara hiyo ni tusi baya haswa, ni sawa na kuonyesha kidole cha kati juu (up yours) nchini Marekani.
- *Pesa*: Kupitisha kidole gumba katika kidole cha shahada kwa mwendo wa kwenda nje (ilihali vidole vingine vitatu vimekunjwa) mfano wa mtu ahesabuye pesa za noti: Hii ni ishara ya pesa.
- *Kuhesabu mpaka tano*: tunapohesabu mpaka tano; ni kaida kuanza na kukunja ngumi na kisha kukunjua kidole kimoja kimoja kuanzia kidole cha mwisho, kuja kidole cha pete, halafu cha kati, kisha cha shahada na kumalizia na kidole gumba na hivyo kufanya kiganja kuwa wazi tunapomaliza kuhesabu mpaka tano.
- *Kidole cha shahada* hutumika kujielekezea kifuani aghalabu upande wa kushoto hii ni ishara ya kuonyesha nafsi ya mtu yaani "mimi" pia hutumika kuonyeshea mahali kama "hapa" au "pale" na kuonyesha vitu.
- *Kushika tama* yaani mtu kuegemeza shavu katika kiganja chake hususan akiwa ameketi ni ishara ya huzuni/majonzi au mawazo hasa unapokuwa na jambo linalokutatiza. Ikiwa mtu atakuona umeshika tama huenda akakuuliza vipi una nini mbona umeshika tama?
- *Kupunga mkono*: kutikisa mkono kulia na kushoto kwa kurudia rudia kiganja kikiwa wazi na aghalabu juu kidogo ya mabega ni ishara ya kuaga "kwa heri" au kumsalimu mtu aliye mbali kidogo nawe. Ilhali kupunga mkono chini ya mabega huweza kufasiliwa kuwa ni ishara ya kukataa "hapana", hili hutegemeana na muktadha wenyewe.
- *Alama ya tiki* (tick): Alama ya tiki ni ishara chanya ina maana ya "ndiyo, sawa, au umepata jibu sahihi ". Ni kaida kutumiwa na walimu mashuleni wanaposahihisha kazi za wanafunzi, pia hutumika katika fomu na hojaji mbalimbali. Pia, mtu huweza kuichora hewani kwa kidole chake cha shahada katika mazungumzo anapotaka kushiria mwenzake amepatia jambo linalozungumziwa. Kwa kulinganisha alama hii huashiriwa na duara dogo mfano wa sifuri katika utamaduni wa Japani na alama ya tiki huweza kuwa na maana ya kukosea. Huu ni mfano wa mkanganyiko wa kimawasiliano unaoweza kutokea kutokana na ishara kutokana na tofauti za kitamaduni.
- *Alama ya kosa* (X): Alama hii ni kinyume cha alama ya tiki na hutumika kuashiria "hapana, si sahihi, au umekosa". Kama ilivyo kwa alama ya tiki, alama hii pia hutumika mashuleni kusahihisha kazi za wanafunzi au tunapojaza fomu na hojaji mbalimbali. Sawa sawa na ile

ya tiki mtu huweza kuiashiria kwa kuchora hewani "x" kwa kidole chake cha shahada.

- *Kupigapiga kidole cha shahada kikiwa wima katika ubavu wa kichwa*; ni kuashiria "akili". Ilhali kuzungusha kidole cha shahada (kikiwa katika ulalo) huku vidole vilivyosalia vimekunjwa na kisha kuashiria kufungua kiganja kuna maana ya "wenda wazimu/kichaa".

### 2.7.2 Ishara Hasi za Mwili

Hapa tunadondoa baadhi ya ishara zenye maana hasi ambazo tunaweza kusema si adabu kuzitumia au hazikubaliki kitamaduni;

- **Si adabu** kabisa *kumwita mtu kwa kidole kimoja* agh. kwa kunyanyua kiganja na kutumia kidole cha shahada katika mwendo wa kukikunjia ndani (beconing gesture), hivyo ni sawa na kumwita mnyama. Ishara hii ina taswira sawa sawa nchini Ufilipino; usimwite mtu kwa kidole, hivyo ni sawa na ishara ya kumwita mnyama kama mbwa.
- **Si adabu** *kuwanyooshea watu kidole* cha shahada iwe ni kwa lengo la kuonyesha au kurudiarudia kumwelekezea mtu kidole hususan watu hufanya hivyo wanapokasirika au kuonya kwa hasira.
- *Kutumia mkono wa kushoto* **si adabu** kabisa. Huashiria mtu kukosa heshima au kuonyesha dharau. Desturi hii ina athari ya dini ya Kiislamu. Kwa kulinganisha si adabu pia kula kwa mkono wa kushoto katika desturi za Kihindi.
- *Kukunja uso* (to frown) *na kufyonya* (to make a hissing sound as a sign of contempt) huashiria dharau, chuki au hasira. Watu husonya na kukunja uso wanapolemewa na hisia za hasira na kukereka, hata hivyo mambo haya **si adabu** kufanya.

## 2.8 Mambo ya Mapenzi, Ndoa na Kujamiiana

Eneo hili lina miiko mingi kitamaduni. Katika tamaduni mbalimbali labda yapo mambo ambayo hayazungumziwi au tuseme hayasemeki hadharani kwa kawaida. Mathalan, katika utamaduni wa Kiswahili **ni mwiko** kuzungumza hadharani kuhusu mapenzi au mambo ya kujamiiana. Pia **ni mwiko** kuonyesha mapenzi hadharani kwa mfano kwa wapenzi kubusiana au kukumbatiana n.k. Pia **ni** jambo la **mwiko** kujihusisha na mapenzi kabla ya ndoa, nje ya ndoa au kuwa na mapenzi ya jinsia moja, kunajisi au umalaya (kujiuza). Zaidi **ni mwiko** kwa ndugu wa damu kuoana. Mambo haya kwa kiasi kikubwa yana athari ya dini hasa dini ya Kiislamu, kama tulivyojadili katika makala iliyotangulia (Isack 2020: 194-199), maisha, tamaduni na desturi za Waswahili zimefungamana sana na dini ya Kiislamu.

### 2.9 Lugha ya Upole au Tasfida

Yapo maeneo kadhaa katika lugha ambapo wanajamii hutumia tasfida ili kupunguza ukali wa maneno kwa unyeti wa maeneo hayo. Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili Sanifu (2014: 554), "tasfida ni matumizi ya maneno ya adabu au fiche yasiyoibua hisia mbaya au kueleza dhana ambazo maneno yanayoziwakilisha hukera watu yasemwapo". Kwa upande wa Waswahili maeneo hayo nyeti ni pamoja na; mambo ya haja (chooni), maradhi, kujamiiana, viungo vya mwili, mambo ya uzazi na ulemavu. Katika sehemu inayofuatia, tutafafanua zaidi na kutoloea mifano pale inapojuzu na kueleza fikra juu ya mambo hayo kwa kuzingatia kila jambo kama linaangukia katika kaida au mwiko.

#### 2.9.1 Mambo ya Haja, Maradhi na Kujamiiana

**Ni mwiko** kitamaduni kusema moja kwa moja maneno yahusuyo haja kama vile; ninakwenda chooni, ninakwenda kukojoa au kunya. Maneno haya huleta ukakasi kweli kweli masikioni mwa watu ikiwa yatatumika, ni ishara ya kutofahamu na kutoheshimu desturi pia. Ni ustaarabu na **ni upole** kutumia maneno ya kificho/tasfida kama kusema ninaenda uani/ maliwatoni/msalani, au ninaenda kujisaidia badala ya kutaja maneno yenyewe ya haja.

Pia **ni jambo la mwiko** kuzungumzia hadharani au kujitaja ikiwa una maradhi kama Ukimwi, na magonjwa ya kuambukiza kwa njia ya kujamiiana kama kisonono au yale ya kuhara kama kipindupindu. Maradhi kama haya huchukuliwa kama ya aibu na pia vile yanagusia/yanahusisha sehemu za siri. Eneo hili ni moja ya yale yenye tasfida na misimu mingi. Unaweza kusikia majina yasiyo rasmi watu wanapozungumza kama fulani ana "ngoma/miwaya/ngwenge" wakimaanisha mwathirika wa ugonjwa wa Ukimwi. Au watu hutumia maneno kama "ugonjwa wa sehemu za siri" badala ya kutaja jina lenyewe la ugonjwa kama "kisonono au kaswende". Pia, unaweza kusikia misimu kama "ninaendesha"/ "nimepoteza ufunguo"/nimepoteza kizibo" (si rasmi) badala ya kutaja moja moja ugonjwa wa kuhara.

Zaidi **ni mwiko** kutumia maneno yanahusiana na kujamiiana moja kwa moja. Aghalabu maneno yasiyo ya moja kwa moja kama; tendo la ndoa, kufanya mapenzi, au utasikia fulani anatembea/anatoka na fulani, ili mradi tu huwezi kutumia maneno yenyewe moja kwa moja.

#### 2.9.2 Viungo vya Mwili na Uzazi

**Ni jambo la mwiko** kutaja majina ya sehemu za siri moja kwa moja kama vile; matako, matiti, majina ya uke au uume wa mwanadamu hasa katika mazungumzo ya kila siku. Badala yake **ni upole** kutumia tasfida yaani kutotaja moja kwa moja au kutumia maneno ya kificho unapotaja majina ya viungo vya siri kwa mfano kusema makalio, kifua, tupu ya mbele/nyuma, sehemu za

siri za mwanamke au mwanamume, kwa bibi au kwa mjomba au kutumia maneno ya ishara tu/kuonyesha kama kusema "huku chini" ikiwa pana haja sana ya kutaja sehemu hizo mathalani kama upo kwa daktari.

Pia **si upole** kutaja maneno yanahusiana uzazi moja kwa moja unapowarejelea watu mathalan kusema fulani "amezaa" au fulani ana "mimba". Bora kutumia maneno ya upole kama kusema fulani "amejifungua au amepata mtoto", fulani ni "mjamzito". Hata hivyo **ni kaida** kutumia maneno ya kuzaa na mimba ikiwa tunarejelea wanyama. Unaweza kusikia mbwa wangu amezaa, hii inakubalika na ndiyo kawaida.

### 2.9.3 Ulemavu

**Si upole** kutaja jina la ulemavu wenyewe unapowarejelea watu wenye ulemavu wa aina fulani kama vile "kipofu, kiziwi, kilema, bubu, zeruzeru, kichaa". Badala ya maneno hayo **ni upole** kusema; "wasioona" badala ya vipofu, "albino" badala ya zeruzeru, "watu wenye mahitaji maalum" badala ya vilema, au "watu wenye matatizo ya akili" badala vichaa n.k.

## 2.10 Maneno ya Kuonyesha Hisia ya Upole au Huruma

**Ni upole** kutumia maneno kama; "asante, karibu, samahani, tafadhali, ninaomba, pole" n.k. Hapa tutafafanua kwa kifupi muktadha wa matumizi ya kila moja.

Neno *asante* hutumika tunapoonyesha shukrani kwa mfano mtu anapokusaidia jambo, mtu anapokukaribisha chakula, kinywaji, nyumbani kwake n.k. Zaidi neno hili hutumika kitamaduni kama namna ya kukataa jambo kwa upole. Mathalan, mchuuzi anapokushawishi kununua bidhaa yake, unaweza tu kumjibu "asante, siku nyingine". Kwa namna hiyo unakuwa umempa ujumbe kama hutaki kununua bidhaa husika lakini kwa namna ya upole.

Neno *karibu* hutumika agh. na mwenyeji, mhudumu au muuzaji kumwalika mtu mahali kama nyumbani kwa mfano; mgeni anapobisha hodi! mwenyeji wake atamjibu "karibu, ingia ndani". Au mteja anapoingia sehemu ya biashara kama vile dukani, sokoni au mkahawani n.k. mhudumu/muuzaji anaweza kumwambia "karibu, nikusaidie nini?", naye mtu anayekaribishwa hujibu kwa kusema "asante".

*Samahani* ni neno wanalotumia Waswahili kwa namna mbili; kwanza ni pale mtu anapoomba radhi kwa jambo alilokosea lina maana sawa na nisamehe au niwie radhi, kumradhi kwa jambo/mambo niliyokosea. Pili, neno hili hutumika pale mtu anapotaka kuvuta usikivu wa mtu/anapotaka mtu awe na makini na lile analotaka kumwambia mtu/watu. Unaweza kusikia kama "samahani dada, unaweza kunielekeza soko kuu la Kariakoo".

Maneno; *tafadhali* na *ninaomba* hutumika sana kuonyesha upole pale tunapokuwa na haja,

tunapotoa maelekezo, tunaposisitiza au tunapotaka kupewa huduma sehemu kama dukani au mkahawani. Unaweza kumsikia mtu akiagiza dukani; "*naomba* mayai manne na mkate mmoja", au mtu akitoa maelekezo/msisitizo; "*Tafadhali* sana umalize kazi yako kufikia wiki ijayo".

Pia **ni kaida** kusikia maneno kama *pole! jamani*! *masikini!* n.k. Neno kama pole hutumika kumwambia moja kwa moja mtu ikiwa mtu atasema kama anaumwa, amechoka au amepatwa na matatizo, msiba au maafa. Sawa sawa na pole neno *jamani!* au *masikini!* ni maneno yanayotumika kuonyesha hisia ya masikitiko au huruma kwa mtu mwingine kwa lile lililompata kama ugonjwa, msiba, ajali, kupoteza mali n.k.

### 2.11 Mavazi

Kipengele hiki kimejalidiwa kwa urefu zaidi katika makala iliyotangulia *Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi* (Isack 2020: 202-204). Hapa tutarudia kutaja kwa ufupi tu mambo ya adabu za mavazi kwa upande wa wasichana/wanawake na wavulana/wanaume.

Kwanza, **si adabu** kwa msichana au mwanamke kuvaa nguo inayoonyesha sehemu kubwa ya mwili wake. Kwa desturi za Kiswahili zenye athari ya dini ya Kiislamu, mtoto wa kike sharti ajistiri mwili wake kwa mavazi yanayofunika sehemu kubwa ya mwili wake isipokuwa uso, na viganja vyake vya mikono na miguu, mavazi ya heshima pia ni yale yasiyobana na kuonyesha umbile lake.

Kwa upande wa wavulana au mwanaume **si heshima** kujipodoa, au kujipamba kwa vito na hasa vile vilivyotengenezwa dhahabu, kuvalia mavazi ya hariri, kusuka nywele, kuchora hinna yote haya huchukuliwa kama **ni kaida** na mapambo ya kike na hayafai au si sehemu ya hulka ya mwanamume kwa mujibu wa desturi za Kiswahili. Vilevile, **si adabu/si heshima** kuvaa suruali chini ya makalio (maarufu kama *mlegezo*), kuvaa kofia (cap) unapozungumza na mtu mzima/mzee/mtu unayemuheshimu au unapokuwa katika sehemu rasmi kama shuleni, au kazini.

## 3. Hitimisho

Mwanzoni mwa makala hii tumetambulisha kuwa makala hii imelengwa kwa wakufunzi na wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni ili kuziba mwanya wa maarifa na uhaba wa rejea zinazowalenga makundi tajwa kuhusiana na lugha ya Kiswahili na Utamaduni wake.

Makala hii imezungumzia mambo ya *Kaida* na *Miiko* kwa kuzingatia vipengele anwai vya maisha katika Utamaduni wa Kiswahili. Kwanza tumeeleza kuwa kila jamii ina seti ya mambo ambayo yanakubalika; mambo ambayo ni desturi, yanayofaa kimaadili, mambo ambayo ni vizuri kuyafanya au kuyasema yote haya tumeyaweka katika kundi la *Kaida* kwa upande mmoja. Kwa upande mwingine kuna mambo ambayo si desturi, si heshima, si vizuri kabisa kuyasema au

kuyafanya haya tumeyaweka katika kundi la *Miiko*. Kisha tumedondoa mambo hayo, na kubainisha namna kila moja linavyofikiriwa kwa kuzingatia makundi hayo mawili. Pia utajirisho wa utamaduni juu ya mambo yaliyotajwa umetolewa pale inapojuzu.

Makala hii ni mwendelezo wa juhudi za mwandishi kuangazia vipengele mbalimbali vya utamaduni wa Kiswahili kwa mahitaji ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni. Kama tulivyokwisha kutaja katika makala zilizotangulia, mtu anapojifunza lugha ya kigeni pia anajifunza utamaduni wa lugha husika. Na kuwa kujifunza utamaduni ni muhimu sana ili kuweza kufahamu, kuwasiliana, kutangamana na kuishi vyema na watu wa jamii ya lugha husika. Hata hivyo bado tunaendelea kutoa wito wa kuongeza rejea zaidi kwa vipengele vingine vya utamaduni wa Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla kwani kama tujuavyo vipengele vya utamaduni ni vingi na changamani na bado havijapata nafasi ya kuridhisha katika maandiko ya Kiswahili. Miongoni mwa vipengele vinavyohitaji kuangaziwa zaidi katika kazi zijazo ni pamoja na; mambo ya lugha, fasihi, sanaa na burudani.

## Marejeo

Isack, Zainabu Kassu

2018 “ Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili”, katika *Frontier of Foreign Language Education 1, 105-118.*

2019 “ Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili”, katika *Frontier of Foreign Language Education 2, 259-269.*

2020 "Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi", katika *Frontier of Foreign Language Education 3, 193-205.*

2001 *Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza* (Toleo la kwanza), TUKI, Dar es Salaam.

2014 *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Tatu), Oxford University Press, Nairobi.